

## **Kiswahili na Ushairi: Dhima ya Upya wa Kiutunzi**

*Kemboi Keitany, Mwanakombo Noordin na Mosol Kandagor  
Chuo Kikuu Cha Moi, Kenya*

### **Ikisiri**

Kiswahili, kama malighafi ya fasihi, kimekuwa na uwezo wa kuibua upya utunzi wa ushairi wa Kiswahili. Upya huu unaenda sambamba na mabadiliko na hatua zinazopigwa na jamii kadri ya mpito wa wakati. Ni upya unaozidi kunawirisha sanaa ya ushairi wa Kiswahili kiuajumi na kiumbuji. Na tunapoangazia upya wa kiutunzi tunazungumzia lugha kama kiungo hai kinachoakisi miktadha halisi ya kihistoria. Licha ya miktadha hii kuathiri mawasiliano ya kawaida ya kila siku ya kisiasa, kiuchumi na kijamii, inaathiri pia usanii wa kifasihi. Usanii huu wa kifasihi unahusu viambajengo vya kimatini hasa mitindo ya uwasilishaji jumbe. Mitindo hii hudhibitiwa na vipashio vya kimofonolojia, uradidi wa vipashio vya kiisimu na maumbo badalia ya kileksia yenye uamilifu wa kisintaksia na wa kisemantiki. Uamilifu huu ndio unaoupa ushairi wa Kiswahili upekee wa kiuajumi na kiumbuji. Kwa jinsi hiyo, makala haya yanachunguza suala la upya wa kiutunzi kidaikronia katika ushairi wa Kiswahili. Lengo ni kudhihirisha nafasi na uamilifu wa Kiswahili katika kuibua maumbo na mitindo mipya katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili.

**Maneno Muhimu:** Kiswahili, Ushairi, Dhima, Kiutunzi

### **Utangulizi**

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu. Historia hii haihusu yaliyomo tu, bali pia mtindo wa uwasilishaji jumbe. Yaliyomo (maudhui) na mtindo huibuliwa kwetu kupitia lugha (katika muktadha huu Kiswahili) kama nyenzo kuu ya uwasilishaji. Kiswahili kimechangia pakubwa katika utunzi, uhifadhi, usambazaji na urutubishaji wa ushairi wa Kiswahili. Urutubishaji huu ndio ambao umeibua na unazidi kuibua upya wa kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili. Kwa jinsi hiyo, makala haya yanawania kudhihirisha jinsi Kiswahili kimeweza kuchipuka kwa upya wa kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili kadri ya mpito wa wakati.

## Ushairi wa Kiswahili

Mulokozi (1974), anadai kuwa ushairi wa Kiswahili ni ule ushairi, andishi au simulizi, ambao unazalishwa kwa Kiswahili na watu wa Afrika Mashariki. Ushairi wa Kiswahili basi ni mpana na hutofautiana katika vipengele vya kiumbo na kimaudhui. Ushairi wa Kiswahili huweza kutambuliwa kupitia vitambulishi vyake vya kihistoria, lugha inayotumiwa, na jumbe za kijamii na kitamaduni zinazopitishwa. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa upya wa kiutunzi unaakisi miktadha ya kihistoria ya jamii, jinsi lugha inavyosukwa ili kukidhi mahitaji ya kijumui na kiumbuji, na jinsi jumbe zinavyobadilika kadri jamii inavyobadilika.

Upekee wa ushairi wa Kiswahili unatokana na jinsi lugha inavyotumiwa kiufundi. Hii ni kwa sababu ushairi, kinyume na riwaya au tamthilia, hujikita katika iktisadi ya lugha. Yaani, ushairi hutumia maneno machache<sup>1</sup> katika jitihada za kuusawiri ulimwengu na malimwengu yake. Na kama asemavyo Shitemi (2010), ushairi ni sanaa ya lugha. Upekee wa ushairi hutokana na jinsi ambavyo lugha inatumika ili kudhihirisha upekee wa umbo na nafsi katika muktadha wa sajili na arudhi za kishairi. Matumizi ya lugha kiumbuji na kiumbo yanayogusiwa na Shitemi (2010), yanahusisha uteuzi wa kimakusudi wa maneno na upangaji wake katika (u)tungo. Ni upangaji unaokusudiwa kuibua mahadhi na midundo maalum inayochomoza upekee wa kisanii, na muhimu zaidi, upekee wa kisajili.

Arege (2013) anasema kuwa kufikia hii leo, ushairi wa Kiswahili umepitia hatua mbalimbali za maendeleo. Kuna mitindo ya awali zaidi yenye kujikita katika kanuni za kiarudhi na kuna mitindo ya baadaye ya washairi kuzivua kanuni hizo. Tofauti hizi za kimtindo zilizaa kile kilichojulikana kama mgogoro wa ushairi<sup>2</sup> katika miaka ya 1970 na 1980. Aina zote mbili za ushairi zimeshuhudia mabadiliko mengi. Mabadiliko haya yanaonesha kuwa sanaa huchukua mikondo mipya kila uchao. Mikondo hii mipya anayozungumzia Arege (2013) inatokana na athari za kimtagusano za kijamii, kiusomi au za kiteknolojia. Indede (2011), anashadidia hali hii anapohoji kuwa sanaa ya ushairi najisawiri kama nyenzo muhimu katika maendeleo na ukuaji wa binadamu ulimwenguni. Mtunzi wa ushairi hupata ilhamu na tajiriba zake kutokana na mitagusano na mivutano ya mijadala ya kimaendeleo inayotokea katika nyakati zake. Maelezo haya yanashadidia ile hali kwamba kadri jamii inavyopiga hatua katika nyanja mbalimbali, utanzu wa ushairi nao hukua ili kuakisi mabadiliko na maendeleo ya kijamii.

---

<sup>1</sup> Mohamed (1984), anasema kuwa ni maneno mateule machache yaliyofinyangwa kisanaa.

<sup>2</sup> Mgogoro huu unaangaziwa kwa kina katika Ngugi, P. (1997). *Mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. (Haijchapishwa).

Ushairi wa Kiswahili wa sasa unakua kulingana na mikondo mitatu mikuu (Frolova 2007). Wafuasi wa mkondo wa kwanza (Wanamapokeo) wanashikilia maumbo ya ushairi wa jadi. Kwa kufuata kanuni za sanaa ya ushairi wa Kiswahili, wanamapokeo wanaendelea kujikita katika mipaka ya tanzu mbili kuu za fasihi ya Kiswahili ya kale, *tenzi* (tendi) na *mashairi*. Utenzi una muundo wake: ubeti huwa na mishororo minne yenye mizani **8** (wakati mwingine **11**). Silabi ya mwisho ya mishororo mitatu mitatu ya kwanza hufanana na ndiyo *kina*, silabi ya mwisho ya mshororo wa nne huitwa *kikomo* na huwa sawa katika utenzi mzima. Hata hivyo, kinyume na madai ya Frolova (2007), silabi ya mwisho ya mshororo wa nne katika utenzi huweza kubadilika.

Katika *mashairi*, mkondo uliozoeleka ni ule wa mshororo mmoja kuwa na mizani **16** na huwa na vipande viwili. Silabi ya nane katika kipande huunda *kina* lakini katika mshororo wa mwisho huweza kuwa tofauti. Hii leo ni nadra kwa Wanamapokeo kutumia *tenzi* ambazo huwa ni ndefu huku wakipendelea umbo fupi- *mashairi*, *ngonjera* na mchanganyiko wa maumbo. Ni vigumu kusema ni kwa nini watunzi walipoteza hamu ya kutumia tenzi ambazo zilikuwa maarufu miongoni mwa watunzi (Frolova 2007). Baada ya maumbo ya jadi kutawala kwa muda mrefu, umbo fupi lilipendelewa ili kuenda sambamba na mabadiliko hayo ili kudhihirisha mawazo na mitazamo ya kizazi kipya barani Afrika.

Katika ushairi wa Kiswahili, mabadiliko ya kiutunzi yaliwakilishwa na kundi la watunzi chipukizi wa miaka ya 1970 waliopinga kanuni za jadi. Hali hii ilipelekea kuibuka kwa mkondo wa pili wa ushairi wa Kiswahili- ushairi wa kisasa. Miongoni mwa waasisi wa “usasa” katika ushairi wa Kiswahili ni Watanzania Euphrase Kezilahabi, Mugyabuso Mulokozi, na Wakenya Alamin Mazrui na Kithaka wa Mberia ambaye anatumia maumbo ya kimajaribio. Kando na Wanamapokeo na Wanausasa, kuna mkondo wa tatu wa ushairi wa Kiswahili- ile namna ya utunzi wa mashairi ambayo inaweza kuitwa ni ya “mpito” (Frolova, 2007). Kwa jumla utunzi huu unaonekana kama “usasa” ambapo kwa kuangalia tu, mtu hawezi kuona mfanano wowote na mashairi ya kiarudhi. Hakika ikichunguzwa kwa undani, ni wazi kwamba kuna mfungamano baina ya sanaa ya kimapokeo na ile ya kisasa. Katika makala haya, mashairi kama haya yameitwa mashairi ya “*aruhu*”, yaani ni mashairi ambayo yanadhihirisha sifa za kiarudhi na zile za mashairi huru. Watunzi wa mashairi ya “*aruhu*” hawapingi kabisa mashairi ya kimapokeo bali wanajaribu kuyapa sura ya usasa, kuyaumba upya kimaudhui na kiumbo, kufanya mabadiliko katika arudhi (vina, mizani) n.k.

Mfano mzuri wa uundaji upya wa ushairi wa kimapokeo ni ushairi wa Said Ahmed Mohamed. Analiunda upya shairi la kimapokeo na kulifanya kuwa la kisasa. Kwa mfano, katika shairi *U Wapi Mpaka?* tunaweza kuona uwepo wa arudhi lakini uundaji upya unatawala. Kwa kungalia tu mara ya kwanza, shairi hili ni la kisasa na halina uhusiano wowote na shairi la kimapokeo:

**Mf 1:**

*Baina ya kuona na kutoona*

*U wapi mpaka?*

*Baina ya maana na liso maana*

*U wapi mpaka?*

(...) (*Kina cha Maisha 1984:34*)

Katika ubeti huu wa kwanza wa shairi *U Wapi Mpaka?* kuna sifa za usasa na za umapokeo. Ni la usasa kwa sababu halina ulinganifu wa mishororo, yaani mingine ni mifupi na mingine ni mirefu kimizani. Shairi hili pia halina mtiririko wa vina. Hata hivyo, shairi hili likipangwa upya linadhihirisha umapokeo. Mishororo ikipangwa upya shairi hili linakuwa la *tathnia*.

**Mf 2:**

*Baina ya kuona na kutoona, u wapi mpaka?*

*Baina ya maana na liso maana, u wapi mpaka?*

(...)

Katika muundo huu, kuna *kina* cha kati *-na* na cha mwisho *-ka*. Aidha, shairi lina mizani **12**(ukwapi) na **6** (utao) katika kila mshororo. Kwa hivyo, mtunzi anavunja muundo wa shairi la kimapokeo ili kuibuka na muundo mpya. Ushairi ulioundwa upya unaonesha mabadiliko ya kanuni za kisanii lakini pia ni tukio la kihistoria na kitamaduni linalodhihirisha mikondo ya kitamaduni na kiujumi ya watunzi wa Afrika Mashariki.

**Lugha ya Kishairi**

Crystal (1987) anasema kumekuwa na hali ya kutoelewana kuhusu lugha ya kishairi. Kwa wengine, lugha ya kishairi ni sharti iwe ya kipekee, iwe tofauti na lugha ya kawaida ya kila siku. Kwa wengine, ni sharti iwe imekaribiana sana na lugha ya kawaida ya kila siku. Kwa upande mmoja, kuna mashairi ambayo yamejitenga sana na lugha ya kila siku, na kwa upande mwingine kuna mashairi ambayo kama haingekuwa mgao katika mishororo, yangepanana na nathari. Midhihiriko ya kishairi huzunguka pande hizi mbili wakati watu wanadhihirisha mivutano ya kiisimu ya jadi na ile ya uhalisia wa kisasa.

Ubunifu ambao washairi huwania huchukua maumbo mengi (Crystal, 1987). Huweza kuhusisha uvumbuzi wa sifa mpya za kiisimu kama vile za kimsamiati au za kitipografia. Lakini wakati mwingi huchukua umbo la utumizi mpya wa lugha ya kawaida. Washairi hujaribu kuepukana na kile ambacho hakipendezi kiisimu au kinachoweza kutabirika, na kuvumbua njia ambazo kwazo maneno huweza kuwa hai ili kuwasilisha dunia mpya za maana. Sifa mbalimbali za kimtindo za kifonetiki na kifonolojia zinachangia katika kuibua athari ya kishairi. Vipande sauti huweza kutumiwa kionomatopoea kwa minajili ya uwasilishaji. Kwa kurudiarudia irabu au konsonanti katika viwango tofauti, maneno na virai huweza kuunganishwa kwa

minajili ya athari za kiuajumi. Huwapo na sauti zenye midundo maalum na pengine maneno kurudiwarudiwa ili yaweze kudhibiti maana inayokusudiwa na mtunzi (Ruo 1989). Kwa jinsi hiyo, tunaweza kudai kwamba uradidi wa vipashio vya kiisimu huhusishwa zaidi na utanzu wa ushairi. Ni uradidi ulio na uamilifu wa kiuajumi na kiumbuji. Aidha, uradidi huu unakusudiwa kukoleza jumbe zinazowasilishwa na mtunzi.

Halliday (1993) anasema, ikiwa tunataka kuchunguza lugha ya kazi fulani ya kifasihi ambayo inatuathiri kama wasomaji, basi inabidi tuchunguze athari za kiisimu tukizihusisha na majukumu ya lugha ambayo yameangaziwa katika kazi fulani. Tanzu mbalimbali za fasihi katika vipindi tofauti vya kihistoria zinatofautiana kimsisitizo katika majukumu mbalimbali ya lugha. Madai haya ya Halliday (1993) yanaashiria kuwa ufasiri wa lugha katika matini za kifasihi hutegemea miktadha ya kihistoria na kijamii. Hali hii inadhihirika wazi tunapolinganisha tungo za jadi na zile za kisasa. Tungo za jadi zilitungwa kwa lahaja za kimaeneo ilhali nyingi ya tungo za kisasa zinatumia Kiswahili sanifu (Kiunguja) ingawa kuna idhini ya matumizi ya lahaja nyinginezo. Mwandishi anaweza kutumia onomatopoea; uteuzi wa maneno ambayo yana midundo sawa ya kisauti (Wray na Wengine 1998). Athari zake huweza kuonekana katika uchanganuzi kwa kutumia unukuzi makinifu wa kifonetiki au kifonemiki ili kudhihirisha sifa zinazofanana za sauti. Aidha, uchanganuzi wa kileksia wa mtindo utahusu uchunguzi wa sababu za kuteuliwa kwa maneno fulani na wala siyo mengine. Utahusu pia uchunguzi wa vidokezo vya kisemantiki vinavyohusu maneno yaliyoteuliwa. Maelezo haya yanamaanisha kuwa mwandishi huweza kuteua (ma)neni fulani kimakusudi ili kuwakilisha dhana au (u)jumbe maalum katika kazi yake. Uteuzi huu huibua suala la usambamba katika ushairi.

Lugha ya kishairi huchota kutoka lugha ya kawaida lakini inapata upekee wake kutokana na jinsi inavyosukwa ili kuibua athari zinazokusudiwa na mshairi. Uhuru alionao mshairi humpa fursa ya kubadili miundo ya kiisimu ya lugha ya kawaida ili kuibuka na upekee wa lugha ya kishairi. Ukiukaji wa kanuni na kaida za kiisimu hupelekea kuwepo kwa lugha inayonata na yenye mguso wa ndani kwa ndani.

Leech (1969) anazungumzia suala la umapokeo au ujadi katika lugha ya kishairi. Anasema, tunaweza kutambua mfanano baina ya fasihi na taasisi nyingine zinazodhihirisha umapokeo katika lugha. Kama ilivyo sheria na dini, fasihi ni uwanja ambamo kumbukumbu za kiisimu za enzi za kale zinahifadhiwa. Vitabu vya kidini na kazi maarufu za kifasihi za jadi ni aina za matini ambazo zinahifadhiwa kwa minajili ya enzi zijazo, neno kwa neno, sentensi kwa sentensi. Si ajabu basi kuwa kudumu kwa lugha ya kale hadi lugha ya kisasa ni sifa ya dhima za lugha zinazokiuka mpito wa wakati. Umapokeo katika fasihi huchochewa na hali ya kutaka kufuata mfano wa mwandishi fulani au kundi la maandishi wa kale. Maelezo haya ya Leech (1969), kimsingi, yanaegemea zaidi katika matumizi ya msamiati wa kale. Ni msamiati ambao hautumiki katika diskosi za lugha ya

kawaida ya kila siku. Kwa mfano maneno kama vile *mtima*, *mboni*, *uwene*, *pulika*, *mangi* n.k. yanatumwa katika ushairi wa Kiswahili. Kwa jinsi hiyo, ushairi wa Kiswahili ni hifadhi muhimu ya historia kuhusu lugha ya Kiswahili, na kama asemavyo Nabhany (1987)<sup>3</sup>, tabia ya Waswahili tangu jadi, mambo yao mengi wamekuwa wakiyahifadhi kwa njia ya tungo na kwa hivyo mila na desturi zao na hata mapisi (historia) yao yanapatikana zaidi katika tungo zao.

### Upya wa Kiutunzi

Upya wa kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili unaenda sambamba na historia na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Kumekuwepo na mabadiliko ya kiutunzi hasa katika mtindo na maudhui kuanzia tungo za jadi hadi tungo za kisasa za karne ya 21. Katika kuangazia upya wa kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili, tunachunguza jinsi Kiswahili kimewezesha kuwepo kwa upya huu. Katika sehemu hii, tutachomoza upya wa kiutunzi kidaikronia ili kuonyesha mabadiliko ya kiutunzi kadri ya mpito wa wakati.

### Tungo za Jadi

Tenzi za jadi zilitoka Uswahilini, hasa pande za Lamu, Pate, Siu na Tikuuni. Huko ndiko walikokuwa wakiishi wengi wa washairi wa tungo za jadi ambazo zinajulikana kwa umaarufu wake. Tungo za jadi katika ushairi wa Kiswahili zilijikita katika tenzi (*Utenzi wa Mwana Kupona*, *Inkishafi*, *Utenzi wa Ayubu*, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* n.k). Njogu na Chimerah (1999) wanaorodhesha sifa za *utenzi* kwa majibu wa wanamapokeo kuwa:

- i. Kimaudhui, *utenzi* ni utungo wenye maudhui yanayosimulia kwa kirefu tukio fulani maalum.
- ii. Una beti nyingi kuliko tungo nyingine za Kiswahili. Hauna mizani nyingi- aghalabu ni mizani **8** kwa mshororo. Ni nadra kuwa chini ya **6** au zaidi ya **12**.
- iii. Mshororo haugawanywi mara mbili (katika vipande viwili). Mishororo yake ni minne kwa kila ubeti, mistari mitatu ya kwanza ikiwa na vina vyenye urari, mistari wa mwisho huwa na kina tofauti.
- iv. Kina cha mwisho katika kila ubeti hakibadiliki.

Nyingi ya tenzi za jadi zinaakisi sifa hizi. Zinasimulia visa kwa urefu na hivyo basi kuwa na beti nyingi. Kwa mfano, *Utendi wa Masahibu* una beti 1070, *Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani* una beti 1000, *Utenzi wa Inkishafi* 77 (inaaminika beti nyingine zilipotea, *Taz Shitemi* 2010), *Utenzi wa Mwana Kupona* 99 (kuna

---

<sup>3</sup>Ni maelezo ya Nabhany katika *Utangulizi wa Malenga wa Karne Moja* (1987)- Shihabudin Chiraghadin.

utata kuhusu idadi kamili ya beti) n.k. Tenzi hizi pia zilizingatia idadi maalum ya mizani huku mishororo mitatu ya kwanza ikiwa na urari wa vina ingawa hutofautiana kutoka ubeti hadi ubeti. Tungo za jadi zinajumuisha tenzi zilizojikita katika mizani 8 katika kila mshororo (huwa minne). Utenzi hauna vina vya ndani kwa sababu huwa na kipande kimoja tu. Kina cha mshororo wa mwisho hurudiwarudiwa katika utungo mzima (Wamitila 2008).

**Mf 3:**

(...)  
Moyo wangu nini huitabiri!  
Twambe u mwelevu wa kukhitari  
Huyui dunia ina ghururi?  
Ndia za tatasi huzandamaye  
  
Suu ulimwengu bahari tesi  
Una matumbawe na mangi masi  
Aurakibuo juwa ni mwasi  
Kwa kulla khasara ukhasiriye  
(...) (Mlamali 1981:69)

Katika mfano huu, kina **-ye** kinapatikana katika utungo mzima wa *Inkishafi*. Mtindo huu unatumika katika karibu tenzi zote za jadi. *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* (kina **-ya**), *Utenzi wa Fumo Liyongo* (kina **-ya**) n.k. Hata hivyo, ingawa tenzi za jadi zilikidhi mahitaji ya mizani 8, baadhi yazo zilipungukiwa katika kuzingatia kinakimoja katika utungo mzima. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Masahibu*, baadhi ya beti zina kina **-a** na nyingine **-ya**, *Utenzi wa MwanaKupona* una baadhi ya beti zenye kina **-ya**, nyingine **-a** na **-wa**.

Watunzi wa baada ya kina *Mwana Kupona* walijaribu pia kutilia maanani mizani na vina katika tungo zao. Kwa mfano, Muhammad Kijumwa katika *Utenzi wa Siraji* anatumia kina **-a** katika karibu beti zote isipokuwa ni tofauti katika baadhi ya beti kama vile ubeti wa 123 na 165 ambapo kuna kina **-ya**. Hata Shaaban Robert anajaribu kuzingatia vina katika *Utenzi wa Hati* na *Utenzi wa Adili* ingawa kuna upungufu wa ulinganifu.

Tenzi siku zote hutumiwa kwa kusimulia hadithi za pahala au za watu ambao ni mashujaa na maarufu (Nabhany 1987)<sup>4</sup>. Vile vile hutumiwa kwa kutolea waadhi au wosia. Yote haya ni kwa sababu tenzi ndiyo bahari ya pekee katika ushairi wa Kiswahili iwezayo kuelezea jambo kwa urefu sana bila ya kumchokesha mtu.

---

<sup>4</sup> Maelezo ya Ahmed Nabhany katika *Utangulizi wa Malenga wa Karne Moja* (1987)- S. Chiraghdin.

Maelezo haya yanapata mifano kutoka *Inkishafi* (unahusu ufanifu na uvunjifu wa Wafalme wa mji wa Pate), *Utenzi wa Mwana Kupona* (unahusu wosia wa Mwana Kupona kwa bintiye Mwana Hashima binti Mataka), *Utenzi wa Fumo Liyongo* (unamhusu shujaa wa Uswahilini Fumo Liyongo) n.k

Tungo zinazohusishwa na Fumo Liyongo kama urithi wa Waswahili ni muhimu sio tu kwa sababu za kitamaduni au historia ya sanaa ya kishairi bali pia kwa sababu ya lugha iliyotumika katika tungo hizi (Miehe na Wengine 2004). Kuna maumbo (bahari) matatu yanayohusishwa na tungo za Fumo Liyongo: *Utumbuizo*, *Ukawafi* na *Utendi*. Katika maana yake pana, *utumbuizo* unarejelea “bembe/Bembelezi” au “wimbo” wowote uliokusudiwa “kutuliza”. Ingawa *Utumbuizo* unadhihirisha baadhi ya elementi za kiarudhi, kimuundo hubadilikabadilika kuliko maumbo mengine ya tungo za jadi. Kwa mfano, mizani na vina katika *Utumbuizo* si lazima kuwe na urari au uwiano ingawa tungo za Liyongo kuna uwiano. Katika *Utumbuizo* wa Liyongo, *vipande* hupimwa katika misingi ya idadi ya silabi. Kwa mfano, kuna mizani **8x10** katika *Utumbuizo wa Uchi* na **8x8** katika *Utumbuizo wa Kumwawia Liyongo*. Mgao wa mishororo hautokani na kuwepo kwa *kina* cha kati kama ilivyo katika maumbo mengine ya kishairi kwa sababu hakuna kanuni ya kina cha kati katika *Utumbuizo*. Hata hivyo, kwa kawaida huwa kuna *kina* cha mwisho kama ilivyo katika *Utumbuizo wa Kikowa*.<sup>5</sup>

*Ukawafi* unakaribiana sana na *Utumbuizo* na *Utendi* (Miehe na Wengine 2004). Idadi ya mishororo katika kila ubeti katika *Ukawafi* hutofautiana kutoka mishororo miwili hadi minne (Shariff 1988 akirejelewa na Miehe na Wengine 2004) au mitano kama ilivyo katika *Takhmisa ya Liyongo*. Ukosefu wa ulinganifu wa mizani katika *vipande* unaonekana kuwa ni njia moja ya kuainisha *ukawafi*. Kwa mfano, kuna mizani **6x4x5** katika *Utumbuizo wa Dhiki* ambapo unaufanya kuwa *Ukawafi*, lakini kwa kuwa haujagawanywa katika beti unaufanya uwe *Utumbuizo* zaidi.

Neno *Utendi* linaonekana pia kuwa na utata. Kwa kuwa tenzi nyingi za Kiswahili zinadhihirisha matendo ya kishujaa, kwengineko zimejulikana kama *ushairi wa kishujaa* (Miehe na Wengine 2004:25). Tukitilia maanani kipengele cha ushujaa, tungo zinazohusishwa na Liyongo kama vile *Utumbuizo wa Dhiki*, *Utumbuizo wa Uchi*, *Utumbuizo wa Uta* n.k. zina uhusiano wa karibu na tenzi nyingine za Kiafrika kama vile *The Epic of Shaka of the Zulu People* na *The Epic of Sundiata of Old Mali*. Maelezo haya yanaonesha utata uliopo kuhusiana na sifa bainifu za utenzi katika ushairi wa kiswahili. Moja ya sifa hizi inahusu urefu wa utungo. Ikiwa utenzi katika ushairi wa Kiswahili ni ndefu, basi tungo

---

<sup>5</sup> Kwa mifano ya tungo zinazohusishwa na Fumo Liyongo, *Taz.* Miehe na Wengine (2004).



zinazohusishwa na Fumo Liyongo haziwezi kuainishwa kama tenzi kwa kuwa ni fupifupi. Kwa jumla, tungo zinazohusishwa na Fumo Liyongo na tenzi za jadi ziliweka msingi bora na tarehe mpya katika makuzi ya ushairi wa Kiswahili.

### Mashairi

Katika ushairi wa Kiswahili wa kabla ya Karne ya Ishirini, tenzi zilifuatwa na mashairi ya kitarbia yenye kufuata kunga maalum za kiutunzi. Mtunzi maarufu wa mashairi ya kitarbia katika kipindi hiki ni Muyaka bin Haji (1776-1840). Utunzi wake ulijikita katika mizani maalum, vina, idadi maalum ya mishororo, vipande, ulinganifu wa mishororo katika beti n.k. Kwa mfano:

#### **Mf 4:**

*Oa kwamba u muozi, uzoeleo kuowa  
Oa mato maolezi, na mboni ukizikowa  
Oa maji maundazi, meupe kama maziwa  
Oa sizi ndizo ndowa, asokuoa ni yupi?*

*Oa ndiwe muolezi, uzoeleo kuowa  
Oa sifumbe maozi, maninga uchiyavua  
Oa uzaze uzazi, kama ulivyojaliwa  
Oa sizi ndizo ndowa, asokuoa ni yupi?*

(...)

(Shitemi, 2010:101)

Abdulaziz (1979) anadai kuwa bila shaka Muyaka ni kielelezo cha upeo wa mabadiliko na maendeleo ya ushairi maarufu wa Kiswahili. Dai hili linadhihirisha upya wa kitunzi uliowekewa msingi wake na Muyaka bin Haji. Muyaka alizua maumbo mapya na kunga mpya katika utunzi wa ushairi wa Kiswahili. Watunzi wa baada yake waliathiriwa na tungo za Muyaka. Hawa ni kama vile Kaluta Amri Abedi, Ahmed Nassir Juma Bhalo na Shaaban Robert.

Mashairi ya Muyaka bin Haji, kando na kunga za kiutunzi, yanadhihirisha ukwasi wa lugha kwa jinsi alivyokuza uamilifu wa vipashio vya kimofonolojia katika umbuji wa kishairi. Shairi **Sili** lina ubinafsi wa kudhihirisha “mchezo wa lugha” kitakriri na kitabdila (Shitemi 2010). Vimiliki vya kileksia na kimofolojia vinawasilisha maana mbalimbali kiumbuji na kimaudhui:

#### **Mf 5:**

**Silihikumbukasilisili**, tapishi**hamiza**  
**Hamizakama** subili, mtama**hagagamiza**  
**Gagamizasihimili**, moyo wangu haweleza  
Kaki zakwe zingaoza, kati namba havisili

**Silihikumbuka *sili, sili* ni mbili *kwangaza***  
***Kwangaza* kucha silali, silali *halishiliza***  
***Lishiliza* ndizi tali, ndizi tali vingakiza**  
Kaki zakwe zingaoza, kati namba havisili

**Silihikumbuka *sili, sili* kuti *hashindiza***  
***Shindiza* siwatambuli, sitambuli *mungapoza***  
***Mungapozasiwambili, siwambili* vingasoza**  
Kaki zakwe zingaoza, kati namba havisili <sup>6</sup>

(...) (Shitemi, 2010:124) [*Msisitizo ni wetu*]

Katika beti hizi, upekee wa mtindo kileksia na kimofonolojia unadhihirika. Kuna msisitizo unaotokana na takriri neno. Kila ubeti unaanza kwa neno ***sili*** na kurudiwarudiwa katika mishororo. Aidha, kuna maneno yanayotumiwa kumalizia na kuanzia mishororo ingawa mengine hupewa maumbo badalia kwa kudondoshwa kwa kipashio cha kimofonolojia. Kwa mfano:

**Hagagamiza** - gagamiza (*ub.1*)

**Halishiliza**- lishiliza (*ub.2*)

**Hashindiza**- shindiza (*ub.3*)

Matumizi ya takriri na maumbo badalia ya kileksia una uamilifu wa kisintaksia na wa kisemantiki. Ni uamilifu unaoupa shairi upekee wa kiujumi na kiumbuji. Mtindo huu unaonekana pia katika tungo za Fumo Liyongo. Mfano mzuri ni katika *Gungu la MnaraMp'ambe* ambapo tunaona “mchezo wa lugha” wenye kutimiza mahitaji ya kimtindo, kisemantiki na kikumbukumbu (Miehe na Wengine, 2004:28):

**Mf. 6:**

Mama nipeka ***haowe, k'aowe*** urembo na shani ungama  
***Haowe*** mnara ***Mp'ambe, Mp'ambe*** uzainiweo hishima  
Na wenye kupamba ***pambato, pambato*** wavele vitindi na k'ama  
Wavete swaifu ***ziembe, ziembanamikili*** mbee na myuma.

[*Msisitizo ni wetu*]

Katika mfano huu, mishororo yote imesukwa kupitia kwa takriri na tabdila, jambo ambalo linazalisha muumano wa kimatini. Hivyo basi, kuwepo kwa mfanano wa kimtindo baina ya tungo za Liyongo na Muyaka kunadhihirisha kuwa mtunzi hauthiriwa na kazi zilizotangulia na utamaduni wa kiutunzi wa kabla yake na wa wakati wake. Watunzi wa baada ya Muyaka walifafanua na kuuendeleza

---

<sup>6</sup> Beti tatu za kwanza zimenukuliwa kati ya sita.

utamaduni wa kiutunzi uliokuwepo kabla ya Karne ya Ishirini. Hawa ni kama vile Shaaban Robert, Kaluta Amri Abedi, Mathius Mnyampala na wengine. Watunzi hawa walizifufua kunga za utunzi na kuzitumia katika tungo zao. Walisisitiza haja ya tungo kukidhi mahitaji ya arudhi kama vile vina na mizani. Kwa mfano, Shaaban Robert anasisitiza suala la vina na mizani katika *Utangulizi* wake wa *Pambo la Lugha* (1966). Aliyechukua jukumu kubwa la kuelezea na kufafanua arudhi za kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili ni Kaluta Amri Abedi. Anaelezea na kuelekeza namna ya kutumia arudhi hizi katika *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Watunzi na wahakiki wa baadaye walishikilia na kushinikiza kutumiwa kwa arudhi hizi kama vile Shihabudin Chiraghdin katika *utangulizi wa Malenga wa Mrima* (1977). Anatetea kunga za utunzi anaposema kuwa mshairi mzuri ni yule ambaye hatalilemaza umbo la shairi akimaanisha kuwa shairi ni sharti liwe na umbo maalum. Umbo hili hutokana na kuzingatwa kwa vina na mizani pamoja na ulinganifu wa mishororo katika beti.

### **Mashairi Huru**

Ushairi huru ni istilahi inayotumiwa kuelezea utunzi wa mashairi ambayo hayajifungi kwenye kaida za utunzi wa mashairi ya jadi. Mashairi huru ni utanzu unaohusishwa na wale waliopata kisomo cha chuo kikuu katika miaka ya 1960 nchini Tanzania. Watunzi hawa walipata elimu ya chuo kikuu na wakatagusana kwa kiasi kikubwa na kazi za kifasihi kutoka tamaduni nyingine (Abdulaziz 1979). Hawa ni Euphrase Kezilahabi na Ebrahim Hussein wote wakiwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam mnamo 1968/1969.

Utangamano katika mifumo mbalimbali ya kielimu ni shughuli ambayo imechangia sana mabadiliko ya umbo la ushairi (Indede 2008). Hii ndiyo sababu tunapata kwamba mielekeo ya kifasihi ya kipindi baada ya uhuru ilivunja umbo la kitamaduni na kufanyia majaribio maumbo mapya ya ushairi. Mtagusano na utangamano anaouzungumzia Abdulaziz (1979) na Indede (2008) ni ule uliowafanya watunzi hawa wapya kukiuka kaida zilizozoeleka katika ushairi wa arudhi. Kwa mfano shairi la kezilahabi, *Kisu Mkononi*<sup>7</sup>

#### ***Mf 7:***

Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja,  
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo  
Siwezi, kama gurudumu nitajiviringisha.  
Mtelemko mkali huu.  
Lini na wapi mwisho sijui.

---

<sup>7</sup> Limenukuliwa kutoka Abdulaziz (1979), *uk 103- 4*.

Mbele chui mweusi, nyuma mwanga  
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu ya dhambi.  
Kisu! Maisha kafiri haya  
Kama kutazama nyuma au mbele  
Ni kufa moyo mzima!

Sasa kama simba- mtu shauri nimekata  
Ya nyuma sana nisijali, ya mbele sana niyakabili  
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka  
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa  
Kila mpigo wa moyo wangu  
Huu mpigo muziki wa maisha.

Shairi hili halijazingatia kanuni ya vina na mizani wala ulinganifu wa idadi ya mishororo. Limetumia raslimali za kiisimu kupitisha jumbe nzito kuhusu maisha ya binadamu. Muhimu ni namna lugha inavyotumiwa kisanii ili kumtafakarisha na kugusa hisi za ndani za msomaji au msikilizaji. Kwa jumla, mashairi huru yamechangia katika kuibuka kwa maumbo na mitindo mipya kama ilivyo katika kazi za watunzi kama vile Alamin Mazrui.

#### Maishairi ya “Aruhu”

Mashairi ya “*aruhu*”<sup>8</sup>, kwa mujibu wa makala haya, ni mashairi ambayo yana sifa za umapokeo na za usasa. Mashairi haya, kwa upande mmoja, yanaelekea kuzingatia arudhi na kwa upande mwingine yanadhihirisha miundo ya mashairi huru. Said Ahmed Mohamed amejaribu kuoanisha aina hizi mbili za mashairi ya Kiswahili. Baadhi ya tungo zake zinaingia katika mkondo huu wa mashairi ya “*aruhu*”. Katika tungo hizi, muundo wa nje unaonyesha kuwa ni mashairi huru lakini kwa muundo wa ndani ni mashairi ya arudhi. Kwa mfano, shairi *Jicho la Ndani (JN, I)* ni shairi huru (umbo la nje) lenye beti mbili. Ubeti wa kwanza una mishororo 18 huku ubeti wa pili ukiwa na mishororo 36. Mishororo hii haijagawanywa katika vipande na mishororo yenyewe hailingani, mingine imeegemea kushoto na mingine kulia:

#### **Mf 9:**

Waona ‘ni cha kuona  
Kwenye mboni za maoni?  
Mwenye jicho la kuona  
Kina juu na angani  
Si huu uliofana

---

<sup>8</sup> Arudhi + huru = “*aruhu*”.

Uzuri us'o kifani?  
Samawi yamemetana  
Na weupe kweupeni<sup>9</sup>.  
(...)

Tunapozingatia muundo wa ndani, tunaona kuwa shairi hili ni la arudhi kwa kuwa kuna ulinganifu wa vina na mizani. Katika muundo wake wa ndani, shairi hili ni la beti nane zenye vipande viwili na kila ubeti una mishororo mitatu:

***Mf 10:***

Waona 'ni cha kuona, kwenye mboni za maoni ?  
Mwenye jicho la kuona, kina juu na angani  
Si huu uliofana, uzuri us'o kifani ?

Samawi yamemetana, na weupe kweupeni  
Mbingu imetulizana, kama sura ya peponi  
Mwanzo na mwisho haina, imekithiri thamani.

Pole imetulizana, doa hutalibaini  
Ila itazame sana, picha kwa jicho la ndani  
Ndani kinafichamana, kingi kingi kisirani!

Tazama ukiiona, milima ya ukingoni  
Na bonde lililo pana, na busati la kijani  
Na nyama wan'olishana, walioko malishoni

Wadogo wal'ojazana, na wakubwa wa pembeni  
Wote wamekitamana, kwa upole wa amani  
Uwatazamapo sana, wamekutana kwa shani

Kama vile 'mepatana, na amani 'mesaini  
Ila 'kitunga maana, utaona wa vitani  
Mwenye nguvu ambana, dhaifu yu mautini

Simba anafukuzana, na paa yu hatarini  
Chui na 'ye atafuna, windo na damu menoni  
Na nyati wanapigana, wao kwa wao mbugani.

Fisi wanasogezana, mafupa wayatamani  
Vumbi linatifukana, mbwa mwitu wa mbioni  
Tai wanakimbizana, na walao mawindoni

---

<sup>9</sup>Mishororo minane imenukuliwa kati ya hamsini na minne.

Kishindo kuangushana, ni kanuni ya mwituni  
Wanadamu huvotana, bunduki zi mkononi  
Amani tena hakuna, 'kiona jicho la ndani!

Katika muundo huu wa ndani, kuna urari wa vina vya kati na mwisho. Aidha, kuna uwiano wa mizani ambapo kila mshororo una mizani **8x8**. Kwa hivyo, katika kubadili mpangilio wa mishororo (kama ilivyo katika diwani), mtunzi anaibua muundo wa Shairi huru. Mfano mwingine wa shairi la "aruhu" ni *Mwanamwari wa Kesho* (JN, 109):

**Mf 11:**

Mwanamwari wa kesho,  
    atatoka vyengine  
        mwembamba au mnene  
Mweusi au mweupe  
Makini au mahepe  
    atatoka huru,  
        mimbani mwa mama'ake!

Mwanamwari wa kesho,  
    atapokewa vyengine  
        mzima au swenene  
mnene au kifefe  
mkofu au kibofe  
    atabimbwa huru  
        ganjani mwa mama'ake!

(...)

Shairi hili lina sifa za mashairi huru kwa sababu mpangilio wa mishororo hauambatani na ule wa kimapokeo. Hata hivyo, muundo wa ndani unadhihirisha kuwa shairi hili lina beti nne:

**Mf 12:**

Mwanamwari wa kesho, atazaliwa vyengine, mweusi au  
    mweupe  
        mwembamba au mnene,  
makini au mahepe  
    atatoka huru, mimbani mwa  
    mama'ake!  
Mwanamwari wa kesho, atapokewa vyengine, mnene au  
    kifefe

mzima au swenene, mkofu au  
kibofe  
atabimbwa huru, ganjani mwa  
mama'ake!

Mwanamwari wa kesho, si mtumwa tena, ingawa ni  
mwanamke  
si mtawa tena, ingawa yu ndani  
mwake  
si mtete tena, ingawa umbile  
lake  
si hawara tena, ingawa hiari  
yake  
si Malaya tena, hata hivyo  
watamke  
Atakuwa huru, usoni  
mwa baba'ake!

Kulingana na muundo huu, beti tatu za kwanza zina idadi sawa ya mishororo huku wa mwisho ukiwa na mishororo sita. Mshororo wa kwanza wa kila ubeti una vipande vitatu huku mingine ikiwa na vipande viwili. Aidha, shairi hili limezingatia vina na mizani. Hizi ni sifa za mashairi ya arudhi. Hata hivyo, katika diwani, baadhi ya mishororo ya ukwapi ndiyo ambayo inaunda sehemu ya mwandamizi katika muundo wa ndani. Pia, mshororo wa mwisho ambao ungekuwa ndio kiitikio umegawanywa kuwa mishororo miwili. Hali hii inapelekea kuwepo kwa shairi ambalo kimsingi ni la arudhi na wakati uo huo kuonekana kama shairi huru.

Shairi *Nilipokuwa Mjinga (JN, 143-144)* ni mfano mwingine wa shairi la "aruhu". Ni shairi ambalo limezingatia vina na mizani ingawa katika viwango tofauti. Mpangilio wa mishororo katika beti sita za kwanza unalifanya shairi hili kuonekana kama shairi huru. Sehemu ya pili, ambayo ndiyo ubeti wa mwisho, ina vipande viwili vyenye urari wa vina na uwiano wa mizani. Kina cha kati ni *-wa* na cha mwisho ni *-na*. Ubeti huu una mizani 6upande wa ukwapi na 8 katika utao. Kuwepo kwa miundo mbalimbali ya mashairi ya arudhi, mashairi huru na mashairi ya "aruhu" katika tungo za Said Ahmed Mohamed kunadhihirisha upevu wa kiutunzi wa mshairi huyu. Hizi ni tungo ambazo, kama anavyodokeza katika shairi *Arudhi (JN, 78)*, zinadhihirisha msimamo wake kuhusu ushairi wa Kiswahili. Anasisitiza kuwa ushairi hauhusu vina na mizani tu, bali ni muhimu kuoanisha maudhui na fani. Tungo za Said Ahmed Mohamed zinamweka mshairi huyu katika kiwango cha kipekee cha utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Ni utunzi ambao

umeufanya Ushairi wa Kiswahili kupiga hatua kubwa katika historia, maendeleo na makuzi yake.

### **Hitimisho**

Makala haya yamedhihirisha kuwa Kiswahili, kama chombo cha uwasilishaji na usukaji wa jumbe, kimwezesha ushairi wa Kiswahili kupiga hatua na kupanua peo za kintindo kadri ya mpito wa wakati. Peo za kintindo zimeelezwa kidaikronia kuanzia tungo za jadi hadi mashairi ya ‘aruhu’. Kuwepo kwa upya wa kiutunzi katika ushairi wa Kiswahili kumechangiwa pia na miktadha ya kijamii ya kiusomi, kimtagusano na kiteknolojia. Aidha, upya huu wa kiutunzi umenawirishwa na kukasishwa na juhudi za watunzi za kutaka kuibuka na maumbo na mitindo mipya katika ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya juhudi hizi zimesaidia katika kuchipuka kwa mashairi (ya ‘aruhu’) ambayo yanahitaji uchunguzi wa miundo ya nje na miundo ya ndani. Kwa jumla, upya wa kiutunzi ambao umeangaziwa katika makala haya umechangia katika kuhuisha na kurutubisha ushairi wa Kiswahili.



## Marejeleo

- Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: KLB
- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: KLB
- Arege, T. [Mhr](2013). *Tunu ya Ushairi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Chiraghdin, S. (1977). *Malenga wa Mrima*. Nairobi: Oxford university Press.
- Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of LANGUAGE*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Frolova, N. (2007). *The 'Renovated' Poetry of Theobald Mvungi and Said Ahmed Mohamed: On Mechanisms of Transformation of Traditional Swahili Verse*. Katika SWAHILI FORUM 14 (2007), uk 5-15
- Halliday, M. A. K. (1993). *Language as Social Semeotic :The Social Interpretation of Language and Meaning*. London : Edward Arnold.
- Indede, F. N. (2008). *Mabadiliko katika Umbo la Ushairi na Athari zake katika Ushairi wa Kiswahili*. SWAHILI FORUM 15 (2008) uk 73-94
- Indede, F. N. (2011). *Mwanamke Angali Tata katika Ushairi wa Kisasa?* SWAHILI FORUM 18 (2011) uk 163-197
- Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman.
- Mberia, K. (1997). *Mchezo wa Karata*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Mlamali, M. (1981). *Inkishafi:Ikisiri ya Muhamadi wa Mlamali*. Nairobi: Longman.
- Miche, G. na Wengine (2014). *Liyongo Songs: Poems Attributed to Fumo Liyongo; Koln: Poetry*. Nairobi: KLB
- Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longman.
- \_\_\_\_\_ (1984). *Kina cha Maisha*. Nairobi: Longman.
- \_\_\_\_\_ (1980). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longman.
- Mulokozi, M. M. (1974). *Revolution and Rraction in Swahili Poetry*. Makala iliyowasilishwa kwa jopo la mjadala kuhusu Ushiri wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Oktoba 1974.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Mbinu na Nadharia*. Nairobi: JKF.
- Robert, S. (1966). *Pambo la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Ruo, K. R. (1989). *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Macmillan.
- Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.

- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix.
- Wray, A. na Wengine (1998). *Projects in Linguistics*. New York: Oxford University Press.